TANGAZO LA SERIKALI NA. 386 lililochapishwa tarehe 2/6/2023

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA
(SURA 415)

# KANUNI

*(Zimeandaliwa chini ya kifungu cha 61(2)(g)(ii))*

## KANUNI ZA UHAKIKI WA SHEHENA ZA MWAKA, 2023

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
LESENI YA UHAKIKI WA SHEHENA

4. Aina za leseni.
5. Marufuku ya kufanya shughuli za uhakiki bila leseni.
6. Vigezo vya kupata leseni ya uhakiki wa shehena.
7. Masharti ya kuzingatia wakati wa uombaji wa leseni.
8. Ada ya leseni.
9. Uamuzi na utoaji wa leseni.
10. Muda wa uhai wa leseni na uhuishwaji wake.
11. Leseni haiwezi kuhamishwa.

SEHEMU YA TATU
HUDUMA ZA UHAKIKI WA SHEHENA

12. Mahali na wakati wa uhakiki wa shehena.
13. Malipo ya huduma ya uhakiki wa shehena.

14. Uthibitishaji na kurekodi uhakiki wa shehena.
15. Aina ya mizigo kwa madhumuni ya uhakiki wa shehena
16. Majukumu ya mwenye leseni.
17. Masharti ya leseni.

SEHEMU YA NNE
KUFUTWA KWA MUDA NA KUSITISHWA KWA LESENI

18. Hatua za kiudhibiti kwa kukiuka masharti ya leseni.
19. Kusimamishwa kwa leseni.
20. Kufutwa kwa leseni.
21. Matokeo ya kusimamishwa au kufutwa kwa leseni.
22. Mawasiliano ya matangazo.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA JUMLA

23. Makosa.
24. Ushughulikiaji wa malalamiko GN. Na. 338 ya 2018

**MAJEDWALI**

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA
(SURA 415)

**KANUNI**

*(Zimeandaliwa chini ya kifungu cha 61(2)(g)(ii))*

KANUNI ZA UHAKIKI WA SHEHENA, 2023

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina

**1**. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Uhakiki wa Shehena, za mwaka 2023.

Matumizi

**2**. Kanuni hizi zitatumika kwa watoa huduma ya Uhakiki wa Shehena.

Tafsiri

**3**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo-

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;

"tozo zilizoidhinishwa" maana yake ni tozo ambazo zimetolewa na kuruhusiwa kutumika na Shirika;

"mkataba wa kazi " maana yake ni mkataba unaoingiwa baina ya mmiliki wa meli ,wakala wa meli, waendeshaji wa bandari na waendeshaji wa bandari kavu au wamiliki wa mizigo kwa ajili ya kufanya biashara ya uhakiki wa shehena;

Sura ya 415 "Shirika" maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli ambalo limeanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria;

"kipimo cha shehena" maana yake ni kipande au kipimo cha shehena kinachorejewa katika agizo la usafirishaji au mkataba wa usafirishaji ambayo inaweza kutofautishwa kwa madhumuni ya uhakiki wa shehena. ;

Sura ya 166 "bandari za maziwa" ina iliyoainishwa kwenye Sheria ya

Bandari;

"leseni" ina maana leseni ya uhakiki wa mizigo inayotolewa na Shirika la Uwakala wa Meli;

"mmiliki wa leseni" maana yake ni mtu aliyepewa leseni na Shirika kutoa huduma za uhakiki wa shehena kwa niaba ya mmiliki wa mizigo na haijumuishi huduma ya uhakiki wa shehena inayofanyika nje ya bandari;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya uchukuzi kwa njia ya maji;

"ripoti ya utendaji kazi" maana yake ni taarifa ya utendaji kazi inayowasilishwa kwenye Shirika kama ilivyobainishwa katika Kanuni hizi;

"bandari" ina maana iliyoainishwa kwenye Sheria ya Bandari;

"bandari ya bahari kuu" ina maana iliyoainishwa kwenye Sheria ya Bandari;

"huduma ya uhakiki wa shehena" maana yake ni huduma za kibiashara za kuthibitisha na kuhesabu mizigo ya mtu binafsi au vitu vilivyochukuliwa wakati wa kupakia au kupakuliwa kwenye meli au wakati wa kujaza mizigo ndani ya au kusambaza mizigo kutoka kwa kasha kuhusiana na mizigo ya jumla, shehena ya wingi kavu, shehena ya maji kwa wingi, shehena, kitengo cha kuorodhesha, wanyama hai, shehena ya kontena, au shehena yoyote iliyoamuliwa na Shirika na inajumuisha utayarishaji wa taarifa za matukio halisi ya meli , uwasilishaji wa taarifa za uhakiki wa shehena kwa sehemu husika na kuweka kumbukumbu za ajali na matukio;

"taarifa za matukio halisi" maana yake ni ripoti inayoorodhesha matukio yote kwa mpangilio wa matukio bandarini kuanzia wakati notisi ya utayari inatolewa hadi wakati wa kumtoa rubani kwenye kituo cha nje;

"bandari" maana yake ni bandari iliyopo baharini au bandari kavu;

"mwendesha bandari" maana yake kampuni inayofanya kazi kama mkandarasi, wakala au mkodishwaji kwa madhumuni ya kutekeleza shughuli za bandari kwenye bandari au bandari kavu.

## SEHEMU YA PILI
## LESENI YA UHAKIKI WA SHEHENA

Aina za leseni

**4**.-(1) Kutakuwa na makundi mawili yafuatayo ya leseni za uhakiki wa shehena:
(a) leseni ya uhakiki wa shehena itakayotolewa katika bandari za bahari kuu; na
(b) leseni ya uhakiki wa shehena katika bandari za kwenye maziwa.

(2) Kampuni iliyopewa leseni ya uhakiki wa shehena itaruhusiwa kufanya shughuli ya uhakiki wa shehena kulingana na bandari iliyoanishwa kwenye leseni.

Marufuku ya kufanya shughuli za uhakiki bila leseni

**5**.-(1) Kampuni haitaendesha huduma za uhakiki wa shehena katika bandari bila kuwa na leseni halali iliyotolewa na Shirika.

(2) Mtu yeyote anayekiuka masharti ya kanuni hii anatenda kosa.

Vigezo vya kupata leseni ya uhakiki wa shehena

**6**.-(1) Mtu atastahili kupewa leseniiwapo mtu huyo:
(a) ni kampuni ambayo asilimia sitini au zaidi ya mtaji wa hisa unamilikiwa na raia wa Jamhuri ya Muungano;
(b) hana kumbukumbu ya ukiukaji wa kanuni za ndani ya nchi na kimataifa za ulinzi na usalama katika sekta inayodhibitiwa; na
(c) si mbia katika kampuni nyingine yoyote inayojishughulisha na wakala wameli, wakala wa ugomboaji na uondoshaji wa shehena, shughuli za bandari na shughuli za meli.

Masharti ya kuzingatia wakati wa uombaji wa leseni.

**7**.-(1) Maombi ya leseni ya kuhakiki shehena yatawasilishwa kwa Shirika kwenye fomu iliyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza, ikiambatana na nakala zilizoidhinishwa za nyaraka zifuatazo:
(a) cheti ya usajili wa Kampuni;
(b) katiba na hati ya uendeshaji wa kampuni;
(c) cheti cha hisa cha mbia wa kampuni;
(d) cheti cha ulipaji kodi;
(e) uthibitisho wa eneo la biashara;
(f) uthibitisho wa sifa za kitaaluma katika uhakiki wa shehena;

(g) hati ya kiapo kwamba kampuni haijatangazwa kufilisika katika kipindi cha miaka miwili iliyopita;

(h) Uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili; na

(i) nyaraka yoyote kwa kadri Shirika linavyoweza kuhitaji

(2) Maombi ya leseni yatawasilishwa kwa njia ya kielektroniki au njia nyingine kama itakavyoelekezwa na Shirika.

Uamuzi na utoaji wa leseni

**8**.-(1) Majibu ya maombi ya leseni yatatolewa na Shirika ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kupokea maombi hayo.

(2) Mkurugenzi Mkuu atawasilisha uamuzi wa Shirika kwa mwombaji kwa kutumia anwani iliyoanishwa kwenye fomu ya maombi au kupitia mfumo wa kielektoniki wa utoaji leseni, ndani ya muda uliotajwa katika kanuni ndogo ya (1).

(3) Pale ambapo Shirika:

(a) limeridhika kwamba vigezo na masharti ya maombi ya leseni yamezingatiwa, Shirika litatoa leseni kwa muombaji katika fomu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu; na

(b) halijaridhishwa na maombi yaliyowasilishwa, litamjulisha mwombaji kuhusiana na kukataa kutoa leseni kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Nne

Ada ya leseni

**9.** Mleta maombi ambaye amekubaliwa na Shirika atalipa ada iliyoainishwa kwenye Jedwali la Pili kabla ya kupewa leseni yake.

Muda wa uhai wa leseni na uhuishwaji wake

**10**.-(1) Leseni iliyotolewa chini ya Kanuni hizi itakuwa halali kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe ya kutolewa, na inaweza kuhuishwa kila mwaka.

(2) Ombi la uhuishaji wa leseni litafanywa katika fomu iliyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza na kuwasilishwa kwa Shirika siku thelathini kabla ya kuisha kwa muda wa leseni iliyopo.

(3) Maombi yoyote ya kuhuisha leseni yanayowasilishwa kinyume na kifungu kidogo cha (2)

yatatozwa ada ya asilimia ishirini ya ada iliyoainishwa.

Leseni haiwezi kuhamishwa

**11**. Leseni iliyotolewa chini ya Kanuni hizi haitahamishwa au kupewa mtu mwingine yeyote.

## SEHEMU YA TATU
## HUDUMA ZA UHAKIKI WA SHEHENA

Mahali na wakati wa uhakiki wa shehena.

**12**.-(1) Huduma za uhakiki wa shehena zitafanywa ndani ya majengo ya bandari au sehemu nyingine yoyote iliyoidhinishwa au kuelekezwa na Kamishna wa Forodha.

(2) Wakala wa meli, mkusanyaji na mtawanyaji wa mizigo, msafirishaji na mmiliki wa mzigo atapaswa kutoa taarifa ya maandishi kuhusiana na mahali na muda ambapo huduma ya uhakiki wa mzigo inafanyika.

(3) Huduma ya uhakiki wa shehena itafanyika-

(a) wakati wa upakuaji au upakiaji wa mizigo wakati meli ikiwa kando; na

(b) iwapo ni upakiaji au upakuaji wa mizigo, kwenye kasha likiwa bandarini au sehemu nyingine yoyote iliyoidhinishwa au kuelekezwa na Kamishna wa Forodha.

Malipo ya huduma ya uhakiki wa shehena

**13**.-(1) Huduma ya uhakiki wa shehena katika upakuaji au upakiaji wa mzigo kwenye meli au upakiaji na upakuaji wa mzigo kwenye kasha linaloshia bandarini gharama zitalipwa na mmiliki wa meli, mbebaji wa mzigo au msafirishaji.

(2) Pale ambapo uhakiki wa shehena unafanywa kwenye mpangilio wa kasha linalotoka nje ya bandari, ada ya uhakiki wa shehena italipwa na mmiliki wa mizigo.

Uthibitishaji na kurekodi uhakiki wa shehena

**14**. Mmiliki wa leseni anayefanya shughuli za uhakiki wa shehena atathibitisha vipimo vya mizigo kama ilivyoainishwa katika orodha ya mizigo, agizo la usafirishaji au matamko ya forodha na kuweka kumbukumbu kuhusiana na-

(a) maelezo ya mzigo;
(b) alama na namba za miigo;
(c) tani;
(d) namba ya kasha, ukubwa na aina;
(e) idadi;
(f) nambari ya lakiri;
(g) vifurushi;
(h) hali yakasha au sehemu za mizigo; na
(i) maelezo mengine yoyote kama itakavyoainishwa na Shirika.

Aina za mizigo kwa madhumuni ya uhakiki wa shehena

**15**.-(1) Huduma za uhakiki wa shehena zitafanywa kwa kuzingatia aina zifuatazo za mizigo:
(a) bidhaa mchanganyiko;
(b) shehena ya wingi kavu;
(c) shehena ya magari na mitambo inayoingizwa na kupakuliwa yenyewe kutoka kwenye meli;
(d) wanyama hai;
(e) shehena ya kontena; na
(f) shehena nyingine yoyote kama Shirika litakavyoainisha.

Majukumu ya mwenye leseni

**16**.-(1) Mmiliki wa leseni chini ya Kanuni hizi atafanya kazi zifuatazo:
(a) kufanya shughuli za uhakiki wa shehena;
(b) kuandaa na kuwasilisha kwa wakala wa meli taarifa ya ukweli wa huduma iliyokabidhiwa na kuwasiliana na kiongozi wa meli kwa ajili ya kusaini taarifa hizo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tano;
(c) kuwasilisha kwa wakati taarifa za uhakiki wa shehena kwa wakala wa meli, idara ya forodha kwa maelekezo na mamlaka nyingine yoyote husika kama Shirika litakavyoelekeza;
(d) kuweka kumbukumbu za ajali na matukio ya mizigo iliyoharibika au kupotea wakati wa shughuli za uhakiki wa shehena; na
(e) kutekeleza majukumu mengine yoyote kama yanavyoweza kubainishwa katika mkataba wa kazi isipokuwa mkataba wa kazi ipo kwenye tasnia ya usafirishaji kwa njia ya meli kwa huduma ya uhakiki wa shehena.

(2) Taarifa za uhakiki wa shehena zilizotayarishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1)(b) zitawasilishwa kwa njia ya kielektroniki au vinginevyo kama itakavyoelekezwa na Shirika.

Masharti ya leseni

**17**.-(1) Mmiliki wa leseni chini ya Kanuni hizi atapaswa:

(a) kutumia ada na tozo zilizoidhinishwa;
(b) kutojihusisha na shughuli za uwakala wa meli, shughuli za meli na ugomboaji na uondoshaji wa shehena;
(c) kudumisha kiwango cha ukwasi cha 2:1;
(d) kuajiri angalau wafanyakazi wawili wenye sifa na elimu ya tasnia ya usafirishaji kwa njia ya maji;
(e) kuanzisha mfumo wa kushughulikia na kutatua malalamiko au migogoro ya wateja;
(f) kuwasilisha katika Shirika taarifa ya utendaji kazi kila baada ya miezi mitatu kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Sita;
(g) kuzingatia kanuni za ushindani kama ilivyobainishwa katika Sheria ya Ushindani wa Haki;
(h) kuzingatia usalama na ulinzi kama ilivyobainishwa katika sheria husika;
(i) kutunza vitabu vya hesabu;
(j) kuvaa sare inayofaa na kitambulisho kama itakavyoelekezwa na mwendeshaji wa bandari;
(k) kutunza rejista ya matukio, na ajali zinazohusiana na huduma zake na hatua zilizochukuliwa;
(l) kuzingatia sheria na kanuni zinazohusiana na uhakiki wa shehena;
(m) kujiepusha na vitendo vya rushwa na ulaghai;
(n) kuzingatia mienendo mingine yoyote ya kitaaluma kama itakavyoelekezwa na Shirika; na
(o) kulitaarifu Shirika kuhusu mabadiliko yoyote ya eneo la biashara au anwani.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni hii, "mtu mwenye sifa ya elimu ya usafirishaji" maana yake ni mtu ambaye ana astashaada katika shughuli za uhakiki wa shehena, shughuli za bandari na shughuli za meli.

## SEHEMU YA NNE
## KUFUTWA KWA MUDA NA KUSITISHWA KWA LESENI

Hatua za kiudhibiti kwa kukiuka masharti ya leseni

**18**.-(1) Shirika, likiridhika kwamba mwenye leseni amekiuka masharti ya leseni yaliyoanishwa katika Kanuni hizi, litatoa adhabu kulingana na uzito wa ukiukwaji kama ifuatavyo:

(a) kumtoza faini;
(b) Kusitisha kwa muda leseni; au
(c) kufutwa kwa leseni.

Kusimamishwa kwa leseni

**19**.-(1) Shirika linaweza kusitisha leseni kwa muda kwa sababu ya mmiliki wa leseni kutofuata masharti ya leseni chini ya Kanuni hizi.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1), kutofuata masharti ya leseni chini ya kanuni ya 17 (b), (c), (d), (e), (f), (g), (i), (j), (k), (l), (n), au (o), kutasababisha kusitishwa leseni kwa muda.

(3) Usitishaji wa leseni kwa muda hautatekelezwa bila kutolewa notisi ya awali inayomtaka mwenye leseni-

(a) kuonesha sababu ndani ya siku ishirini na moja kwa nini leseni isisitishwe kwa muda kwa namna ilivyoainishwa katika Jedwali la Saba; au
(b) kuchukua hatua mahususi za kurekebisha ukiukwaji wowote au kutofuata masharti ya leseni

(4) Endapo mmiliki wa leseni anashindwa kuonesha sababu au kuchukua hatua mahususi za kurekebisha uvunjaji wa masharti yaliyoanishwa kwenye leseni, Shirika litatoa notisi ya kusitishwa kwa leseni kwa muda usiozidi miezi sita na kutoa sababu za usitishwaji huo

(5) Notisi ya kusitisha kwa muda itakuwa katika fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Nane.

(6) Kusitishwa kwa muda chini ya kanuni ndogo ya (4) kutakoma baada ya kuisha kwa muda uliotajwa katika notisi ya kusimamishwa au baada ya kutimizwa kwa matakwa yaliyoainishwa katika notisi ya kusitishwa kwa muda.

(7) Bila kujali masharti yaliyoanishwa katika kanuni hii, Shirika linaweza kutoza faini kutokana na mmiliki wa leseni kutofuata masharti yoyote yaliyoanishwa chini ya

kanuni ndogo ya (2) kama ifuatavyo:

(a) shilingi za Kitanzania laki tano kwa mmiliki wa leseni ya uhakiki wa shehena kwenye bandari ya maji makuu; na

(b) shilingi za Kitanzania laki mbili kwa mmiliki waleseni ya uhakiki wa shehena kwenye bandari ya maziwa makuu.

Kufutwa kwa leseni

**20**.-(1) Shirika linaweza kufuta leseni kwa sababu ya kutofuata masharti ya leseni yaliyoanishwa chini ya kanuni ya 17(a), (h) na (m), kupoteza sifa stahiki au kushindwa kutekeleza masharti yaliyoanishwa chini ya Kanuni hizi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, pale ambapo mmiliki wa leseni anakiuka masharti yanayopelekea kusitishwa kwa muda kwa leseni angalau mara tatu katika kipindi cha uhalali wa leseni, Shirika linaweza kufuta leseni.

(3) Shirika halitafuta leseni isipokuwa kama mmiliki wa leseni amepewa fursa ya si chini ya siku thelathini kuonesha sababu za kwa nini leseni isifutwe kwa namna ilivyoainishwa katika Jedwali la Saba.

(4) Bila kujali masharti yaliyoanishwa chini ya kanuni hii, mmiliki wa leseni ambaye leseni yake imefutwa anaweza kuomba leseni baada ya kuisha kwa miaka mitatu toka ilipofutwa.

Matokeo ya kusimamish wa au kufutwa kwa leseni

**21**.-(1) Pale ambapo leseni imesitishwa kwa muda, mmiliki wa leseni atakoma kufanya kazi ya uhakiki wa shehena kuanzia tarehe ya kutolewa kwa notisi ya kusitishwa kwa muda hadi muda wake utakapoisha.

(2) Pale leseni inapofutwa, mwenye leseni atatakiwa kufanya yafuatayo ndani ya muda wa siku kumi na nne-

(a) kusalimisha leseni ya uhakiki wa shehena kwa Shirika; na

(b) kusitisha kufanya kazi kuanzia tarehe ya kutolewa kwa notisi ya ufutwaji wa leseni.

(3) Notisi ya kusitishwa kwa muda au kufuta leseni ya uhakiki wa shehena itatolewa chini ya kanuni hizi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nane.

Mawasiliano ya matangazo

**22**. Notisi ya kuonesha sababu, kusitisha kwa muda au kufutwa kwa leseni itahesabika kuwa imewasilihwa kwa mmiliki wa leseni iwapo:

(a) itatolewa kwa mmiliki wa leseni au mwakilishi wake aliyeidhinishwa;
(b) itabandikwa katika sehemu ya wazi ya eneo la biashara lililosajiliwa;
(c) itatumwa kwa barua pepe au kwa anwani rasmi ya barua iliyosajiliwa ya mmiliki wa leseni.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA JUMLA

Makosa

**23**.-(1) Mtu yeyote ambaye -
(a) anafanya biashara ya uhakiki wa shehena bila kuwa na leseni halali;
(b) anawasilisha taarifa za uongo wakati wa kuwasilisha maombi ya kuomba leseni ya uhakiki wa shehena;
(c) anawasilisha taarifa, maelezo au kumbukumbu ambazo anajua ni za uongo;
(d) anashindwa kubandika leseni mahali pa wazi katika eneo lake la biashara;
(e) anashindwa kutoa leseni iwapo atatakiwa kufanya hivyo;
(f) anazuia afisa wa Shirika, au afisa mwingine yeyote aliyeidhinishwa katika kutekeleza majukumu yake chini ya Kanuni hizi;
(g) anashindwa kurejesha leseni iwapo ataelekezwa hivyo;
(h) anashindwa kuwasilisha taarifa ya utendaji kazi; na
(i) anashindwa kuzingatia masharti yoyote yaliyoanishwa katika leseni;
(j) anashindwa kutoa taarifa kwa maandishi kuhusu mahali na wakati wa kufanya huduma ya uhakiki wa shehena kinyume na kanuni ya 13(2).

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya shilingi laki tano lakini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi mitano na kisichozidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

Ushughulikiaji wa malalamiko GN.

**24**. Mtu yeyote ambaye hajaridhishwa na na uamuzi wa Shirika chini ya Kanuni hizi anaweza kutafuta nafuu za kisheria kwa mujibu wa Kanuni za Wakala wa Meli

*Tangazo La Serikali Na. 386 (linaendelea)*

Nambari 338 ya 2018 Tanzania (Ushughulikiaji wa Malalamiko).

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA**
**TASAC**

## JEDWALI LA KWANZA

*(Iimeundwa chini ya kanuni 7 (1) and (2) and 10(2))*

### MAOMBI YA LESENI YA UHAKIKI WA SHEHENA

Jina la mwombaji………………………………………………………………………
Anwani ya Posta: ……………………………………………………………………
Namba ya simu…………………………………………………………………...
Namba ya Nyumba/Jengo……………………….
Jina la Mtaa……………………………………..
Msimbo wa Posta………………………………………
Mkoa/ Wilaya…………………………….
Barua pepe:………………………………
Aina ya leseni : Mpya ☐ Kuhuisha ☐

Jamii ya leseni Bandari za maziwa ☐ Bandari kuu

Nambari ya leseni ya awali………………… Mwaka iliyotolewa…………………
Nambari ya Cheti cha Usajili wa Kampuni………………… Tarehe kilichotolewa……………..
Taarifa za wanahisa wa sasa

| JINA | UTAIFA | ANWANI |
|---|---|---|

Tafadhali weka alama kwenye biashara yoyote inayofanywa na Kampuni yako kutoka kwenye orodha iliyo hapa chini:
Wakala wa Meli ☐

Wakala wa Forodha ☐

Shughuli za Bandari ☐

Taarifa ya menejimenti iliyopo sasa na Wafanyakazi wengine

*Tangazo La Serikali Na. 386 (linaendelea)*

| | JINAKAMILI | CHEO/NAFASI | URAIA | UMRI | SIFA | | MIAKA YA UZOEFU | TAREHE YA KUTEULIWA KWA NAFASI YA SASA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ELIMU | UTAALAMU | | |
| 1. | | | | | | | | |
| 2. | | | | | | | | |
| 3. | | | | | | | | |
| 4. | | | | | | | | |

**Tafadhali ambatisha nyaraka zifuatazo wakati wa kutuma maombi:**

(a) cheti cha kuingizwa au usajili;
(b) katiba na hati ya uendeshaji wa kampuni ;
(c) cheti cha nambari ya mlipa kodi;
(d) uthibitisho wa eneo la biashara;
(e) uthibitisho wa sifa za kitaaluma katika huduma za kuhakiki shehena ;na
(f) hati ya kiapo kwamba kampuni haijatangazwa kufilisika katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.

Mimi ………………………………………ninatangaza kwa ufahamu wangu na imani yangu kwamba taarifa na zote zilizomo katika ombi hili ni za kweli na sahihi.

Mimi……………………………………………………… naahidi kuliarifu Shirika iwapo kutatokea mabadiliko yoyote katika umiliki wa hisa na eneo la biashara.

Jina kamili: ………………………………………………………………………

Nafasi/Cheo: ………………………………………………………….………………

Saini: ……………………………………………..… Tarehe:………………

*(Muhuri)*

**KWA MATUMIZI YA OFISI TU**

| **Maoni** | **Kuidhinishwa** | **Kutoidhinishwa** |
|---|---|---|
| | | |
| Tarehe ya kuanza: …………………………….. | | Tarehe ya mwisho wa matumizi…………………….. |
| Namba ya leseni……………………………….. | | |
| Jina:…………………………………………… | | Cheo:……………………… |
| Saini:………………………………………… | | Tarehe:………………………. |

*Tangazo La Serikali Na. 386 (linaendelea)*

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF WORKS AND TRANSPORT**
**TANZANIA SHIPPING AGENCIES CORPORATION**
**TASAC**

## JEDWALI LA PILI

*(Iimeundwa chini ya kanuni 8)*

ADA YA MAOMBI NA LESENI

| Maelezo | Kiasi (Dola) | |
|---|---|---|
| | Bandari ya Bahari Kuu | Bandari ya Maziwa |
| Ada ya maombi | 40 | 10 |
| Ada ya leseni | 500 | 150 |

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA**

**JEDWALI LA TATU**

*(Iimeundwa chini ya kanuni 9(3)(a))*

**LESENI YA UHAKIKI WA SHEHENA**

NAMBARI YA LESENI: …………………………………..…………………………...

Jamii ya Leseni: ……………………………………………..………………………..
M/S:…………………………………………………………………………………………
imeidhinishwa kufanya biashara ya uhakiki wa shehena Tanzania Bara. .
Leseni hii itakuwa hai kutoka
…………………………..hadi…………………………………………….
Ada ya Leseni Dola……………………Imelipiwa kwa stakabadhi nambari. …………ya tarehe…..…………
Ada ya ziada ya maombi ya kuchelewa ya Dola………. Imelipiwa kwa stakabadhi nambari…… …ya tarehe……………………….

………………………………….
Mkurugenzi Mkuu
(Saini na Muhuri)

Tarehe ya kutolewa…………………………………..
**Muhimu:** Leseni hii haiwezi kuhamishwa
Nambari ya mfululizo …………………………………..

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA**

**JEDWALI LA NNE**

*(Iimeundwa chini ya kanuni 9(3)(b))*

TANGAZO LA KUKATAA OMBI LA LESENI YA HUDUMA ZA KUHAKIKI SHEHENA.

Kwenda Kwa …………………………………………………………………

1. Shirika linakutaarifu kwamba ombi lako la Leseni ya Huduma za uhakiki wa shehena chini ya Kanuni za Wakala wa Meli Tanzania (Uhakiki wa shehena ) za 2023 limekataliwa.

2. Sababu za kukataliwa ni:
(a) ……………………………………………………….....................................
(b) ..........................................................................................................................
(c) ..........................................................................................................................
(d) ..........................................................................................................................
(e) ..........................................................................................................................

3. Hata hivyo, maombi yako yanaweza kuangaliwa upya chini ya masharti yafuatayo:
(a) ..........................................................................................................................
(b) ..........................................................................................................................
(c) ..........................................................................................................................
(d) ..........................................................................................................................

Imetolewa tarehe …………………… mwezi wa ..................................... 20.. .............

………………………………….
Mkurugenzi Mkuu
(Saini na Muhuri)

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA**

---

## JEDWALI LA TANO

---

*(Iimeundwa chini ya kanuni 16(1)(b))*

---

### MAELEZO YA CHINI KWA AJILI YA RIPOTI YA TAARIFA YA UKWELI

1. 1.Jina la meli.
2. Nambari ya safari.
3. Bandari ya upakiaji na ushushaji.
4. Wakala wa meli/ mmiliki wa meli.
5. Tarehe na wakati wa chombo kutia nanga.
6. Tarehe na wakati wa kuwasili kwa chombo.
7. Wakati wa taarifa ya zabuni ya utayari.
8. Ucheleweshaji wa saa zinazojitokeza wakati wa operesheni na sababu.
9. Ajali na matukio wakati wa shughuli za uhakiki shehena.
10. Tarehe na wakati wa kuanza kupakuwa mizigo.
11. Tarehe na wakati wa kumaliza kupakua mizigo.
12. Tarehe na wakati wa kuanza upakiaji.
13. Tarehe na wakati wa kukamilika kwa upakiaji.
14. Mizigo kwenye meli (kwa tarehe na zamu).
15. Jumla ya kontena/tani/kifurushi kitakachotolewa na kupakiwa (kwa tarehe na zamu).
16. Tarehe na wakati wa kusafiri kwa meli.
17. Jina, cheo, sahihi ya afisa uhakiki wa shehena aliyetayarisha taarifa na tarehe ya kutayarisha taarifa.
18. Jina, cheo, sahihi ya afisa wa meli aliyeteuliwa ambaye alipokea taarifa na tarehe ya kupokea taarifa.

*Tangazo La Serikali Na. 386 (linaendelea)*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA**

---

## JEDWALI LA SITA

---

*(Iimeundwa chini ya kanuni 17(f))*

---

RIPOTI YA UTENDAJI WA ROBO KWA HUDUMA ZA KUHAKIKI SHEHENA

**SEHEMU YA I: TAARIFA ZA KAMPUNI**

Jina la Kampuni: …………………………………………………………………

Jamii: ……………………………… Nambari ya leseni : …………………….

**SEHEMU YA II: KIPINDI KINACHOTOLEWA TAARIFA**

Kuripoti kila robo mwaka (weka tiki inavyofaa)

☐ ☐ ☐ ☐

Jan-Mach Apr-Jun Jul-Sept Oct-Dis

Jumla ya Meli na mizigo iliyohudumiwa

| **S/N** | **Eneo la huduma (Jina la bandari)** | **Jina la mteja (Wakala wa meli)** | **Jumla ya meli zilizo-hudumiwa** | **Jumla ya tani zilizohakikiwa** | | **Jumla yam akasha yaliyo-hakikiwa** | | **Ro-Ro Units** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mizigo iliyo-ingia | Mizigo iliyo-toka | Mizigo iliyo-ingia | Mizigo iliyo-toka | Mizigo iliyo-ingia | Mizigo iliyo-toka |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |

*Tangazo La Serikali Na. 386 (linaendelea)*

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |

**SEHEMU YA III. MAONI YA JUMLA AU MAELEZO**

i. ……………………………………………………………………………………
ii. ……………………………………………………………………………………
iii. ……………………………………………………………………………………

Jina la muombaji wa Kampuni: …………………………
Cheo: ………………………………………………………
Tarehe: ……………………………………………………… ……………………….
Saini na Muhuri

*Tangazo La Serikali Na. 386 (linaendelea)*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA**

## JEDWALI LA SABA

*(Iimeundwa chini ya kanuni 19(3)(a) and 20(3))*

### TAARIFA YA KUONESHA SABABU

Kwenda kwa………………… mwenye nambari ya leseni :……………………..

Kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi, Shirika linakujulisha kwamba baada ya muda wa siku ……………….. kuanzia tarehe ya kutolewa kwa notisi hii. Leseni iliyotolewa chini ya Kanuni hizi itasitishwa/kufutwa isipokuwa kama, kabla ya kumalizika kwa muda uliotajwa hapa juu, sababu iliyooneshwa kuliridhisha Shirika kwa nini leseni hiyo isisitishwe/kufutwa.

Sababu za kusimamishwa/kufutwa kwa leseni yako:

1. ………………………………………………………………………………………
2. ………………………………………………………………………………………
3. ………………………………………………………………………………………
4. ………………………………………………………………………………………

Imetolewa tarehe……………………… mwezi.................................... 20.. .......................

………………………………….
Mkurugenzi Mkuu
(Saini na Muhuri)

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA**

**JEDWALI LA NANE**

*(Iimeundwa chini ya kanuni 19(4) and 21(3))*

**KUSIMAMISHWA/KUFUTWA KWA LESENI**

Kwenda kwa……………………………………mwenye nambari ya leseni: ……………

Shirika linakutaarifu kwamba leseni yako ya huduma ya kuhakiki shehena iliyotolewa chini ya Kanuni za Wakala wa Meli Tanzania (Uhakiki wa Shehena) 2023, imesitishwa/kufutwa..

Sababu za kusimamishwa/kufutwa:

1. ………………………………………………………………………………………
2. ………………………………………………………………………………………
3. ………………………………………………………………………………………
4. ………………………………………………………………………………………

Imetolewa tarehe ………………………. mwezi......................................20.. ....................

…………………………….
Mkurugenzi Mkuu
(Saini na Muhuri)

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA**

**JEDWALI LA TISA**

*(Iimeundwa chini ya kanuni 24(1))*

**FOMU YA KUFIFISHA MAKOSA**

**SEHEMU YA I: TAARIFA ZA KAMPUNI**

1. Jina la Kampuni…………………………………………………………………….

2. Jamii ya leseni: ………………………………………………….………………

3. Nambari ya leseni:………… imetolewa terehe………inamalizika tarehe……..…

**SEHEMU YA II: UKIRI WA KAMPUNI**

1. Ninakubali kupokea notisi ya kuonesha sababu iliyotolewa tarehe. ................. saa ……………… kuhusiana na kosa lililotajwa hapa chini:
2. ……………………………………………………………………………………
3. ……………………………………………………………………………………
4. ……………………………………………………………………………………

**SEHEMU YA III: KAMPUNI KUKUBALI KOSA KUFIFISHWA**

1. Mimi ……………………………………………………………………………..
nakiri kutenda kosa kinyume na kanuni ……………… ya Kanuni za Wakala wa Meli Tanzania (Uhakiki wa Shehena) 2023

2. Mimi ………………………………… naelewa kwamba kosa/makosa yaliyotendwa yanaweza kufikishwa mbele ya mahakama kwa uamuzi.

3. Ninaomba kosa/makosa yaliyotajwa hapo juu kufifishwa kwa mujibu wa kanuni ………… ya Kanuni za Wakala wa Meli Tanzania (Uhakiki wa Shehena) 2023. Nitalipa faini ya Tshs…………………………… ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya kukiri makosa ikiwa ni jumla ya kiasi cha makosa yaliyofifishwa. Kiasi kilichofifishwa kitalipwa kwa nambari ya akaunti ya benki ya Shirika ………………………………………………

*Tangazo La Serikali Na. 386 (linaendelea)*

Jina: …………………………………………..……………………..……………….
Saini………………………………….......……………………………………..…..
Nambari ya kitambulisho………………...………………………………………

**SEHEMU YA IV: USIPOKUBALI KUWA UMETENDA KOSA(M)JAZA SEHEMU HII**

1. Mimi……………………………………………………………………….. sikubali kukiri kuwa nimefanya kosa kinyume na kanuni……………… ya Kanuni za Wakala wa Meli Tanzania (Uhakiki shehena), 2023.

2. Mimi ……………………………………….. mwenye leseni ya huduma ya kuhakiki shehena nakusudia kujibu Mahakamani shtaka la kutenda kosa ………………………………… ……………………………………………………….. kinyume na kanuni …………………….. ya Kanuni za Wakala wa Meli Tanzania (Uhakiki shehena) 2023.

Jina: ………………………………………………………………………… ………….
Cheo…………………………………………………………………………….…
Saini ………………………………………………………………………….……….
Nambari ya kitambulisho. ……………………………………………...……………..

Dodoma,
18 Mei, 2023

MAKAME M. MBARAWA
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*